JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
Halmashauri Ya Wilaya Ya Mafia
Shule Ya Sekondari Kitomondo

Simu ya mkononi: +225 715520650/+225 625930915
+225 784830018/ +225 652066650

S.L.P 55,
MAFIA.
Tanzania, East Africa

*Kumb.Na. KSS/UC.FV/VOL.01/………..*
……………………………………………………
……………………………………………………

*Tarehe: 22/05/2018*

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO 2018/2019**

Kwa naiba ya bodi ya shule, watumishi na wanafunzi wa shule ya Sekondari Kitomondo, ninapenda kumpongeza mwanao kwa kuchaguliwa kwake kuendelea na masomo ya Sekondari kwa kidato cha tano na kijiunga na shule hii.
Taasusi zilizopo hapa shuleni ni PCB & HGL

***Mahali shule ilipo***
Shule ya Sekondari Kitomondo ipo wilayani Mafiakatika mkoa wa Pwani
Usafiri wa kufika kisiwa cha Mafia unapatikana katika kituo cha mabasi cha mbagala rangi tatu, jijini Dar es salaam. Basi litakufikisha Nyamisati wilaya ya kibiti kwa $Tsh.$ 5,500/= . Kisha Kutoka hapo utapanda boti hadi Kilindoni-Mafia kwa Tsh 16,000/=. Ambapo kuna usafiri wa bajaji kwa Tsh. 4,000/= au pikipiki kwa $Tsh$ 2,000/= kwa umbali wa kilometa tatu hadi shuleni. Muda wa kuripoti ni kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni katika ofisi ya malezi au ofisi ya Mwalimu wa zamu

Au kwa usafiri wa ndege Kutoka terminal one Airport, Dar es salaam hadi Kilindoni-Mafia kwa $Tsh.$ 130,000/=

**MAHITAJI YA LAZIMA KWA KILA MWANAFUNZI**
Ni vyema mahitaji haya yatimizwe kabla ya kuanza safari ya kuja shuleni
**A: Malipo**

i. Karo ya shule kwa mwaka $Tsh.$ 70,000/=au $Tsh.$ 35,000/= kwa muhula
ii. Fedha ya tahadhari (caution money) $Tsh.$ 10,000/=
iii. Fedha kwa ajili ya matibabu $Tsh.$ 20,000/= kwa mwaka au $Tsh.$ 10,000/= kwa muhula, na kwa wanafunzi wenye bima za afya ni vyema waje nazo
iv. Fedha kwa ajili ya kitambulisho cha shule $Tsh.$ 5,000/=
v. Ulinzi na wapishi $Tsh.$ 30,000/= kwa mwaka au $Tsh.$ 15,000/= kwa muhula
vi. Fedha kwa ajili ya uboreshaji wa taaluma kwa mwaka $Tsh.$ 20,000/= au $Tsh.$ 10,000/= kwa muhula
vii. Afike na godoro la futi $3 \times 6$
viii. Mchango wa gharama za umeme $Tsh.$ 10,000/=
ix. Mchango wa samani na ukarabati $Tsh.$ 20,000/= kwa miaka yote miwili au $Tsh.$ 10,000/= kwa mwaka
x. Gharama za kukutumia maendeleo yake kwa kipindi cha miaka miwili $Tsh.$ 5,000/=
xi. Nembo ya shule $Tsh.$ 2,000/=

Malipo yote yafanyike kupitia akaunti ifuatazo
Jina la akaunti: **Kitomondo Secondary Recurrent Account**

A/C NO. **21501200202 NMB**

**NB: HATUPOKEI PESA MKONONI, HAKIKISHA UNAKUJA NA RISTI ZA MALIPO**

**B. SARE ZA SHULE.**

- **WASICHANA.**
  i. Sketi mbili(2) za rangi ya chungwa (orange) hakikisha inakuwa ndefu ya kugusa vifundo vya miguu
  ii. Mashati mawili (2) meupe ya mikono mirefu au brauzi yenye mikono mirefu(Nusu kanzu ndefu na isiyobana) kitambaa cha tetroni na kitambaa cha kichwani(hijabu) ndefu jozi mbili(2) kwa **wanafunzi wa kiislamu**
  iii. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunika miguu jozi mbili(2) vya kamba na vinavyopigwa kiwi **sio vya plastic (Bajaj)
  iv. Soksi nyeupe jozi mbili(2)
  v. Aje na T-Shirt zabluu zenye kola nyeusi ( maarufu form six) na sketi mbili za rangi ya kaki kwa ajili ya kushindia
- **WAVULANA.**
  i. Suruali mbili (2) **dark-blue**zenye mshono wa heshima wa Tanzania (zenye marinda mawili mbele)
  ii. Mashati mawili (2) meupe ya mikono mirefu pamoja na tai mbili (2) za dark-blue
  iii. Soksi nyeupe jozi mbili(2)
  iv. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunika miguu jozi mbili(2) vya kamba na vinavyopigwa kiwi
  v. Mkanda mweusi usio na nembo za kihuni wala bakoli nene.
  vi. Aje na T-Shirt za bluu zenye kola nyeusi ( maarufu form six) na suruali mbili za rangi ya kaki kwa ajili ya kushindia

**NB:**
**Ataripoti shuleni akiwa amevaa suruali/ sketi ya rangi ya kaki na T-Shirt ya bluu**
**Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa suruali mlegezo au ya kubana(modal) akikutwa ataadhibiwa vikali sana ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo**

**C. SARE ZA MICHEZO**

i. Aje na T-Shirt na bukta za rangi ya bluu au tracksuit ya rangi ya bluu
ii. Aje na raba za michezo na vifaa vingine vya michezo

**D: MAAGIZO MENGINE YA SHULE**

i. Cheti cha kuzaliwa na kivuli chake
ii. Cheti cha daktari (medical certificate) cha kuthibitisha afya ya mwanafunzi ambayo itajazwa na hospitali ya serikali
iii. Result slip na kivuli chake
iv. Cheti cha kuhitimu kidato cha nne (leaving certificate) halisi na kivuli chake
v. Picha sita “passport size”ziwe na background za blue awe amevaa shati jeupe
vi. Alete picha moja za passport zize za wazazi au walezi wake wawili
vii. Sanduku imara la kuhifadhia mali zake
viii. Vyombo vya chakula visivyo vya plastiki
ix. Ndoo za plastiki 2 kwa matumizi yake binafsi

x. Aje na chanzo cha mwanga kwa ajili ya tahadhari ya wakati wa usiku iwapo umeme utakosekana
xi. Bunda moja la karatasi (ream A4) kwa mwaka
xii. Scientific calculator kwa taasusi ya PCB ( $fx - 991MS$)
xiii. Dissecting kit kwa wanafunzi wa biolojia na koti jeupe kwa wanafunzi wote wa PCB
xiv. Vitabu vya masomo ya taasusi (combination) husika
xv. Mto wa kulalia
xvi. Shuka mbili za rangi moja (bluu bahari)
xvii. Vifaa vya darasani kulingana na taasusi husika
xviii. Aje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya kazi za usafi
    a. Jembe 1
    b. Panga 1
    c. Kwanja 1

**E: MUHIMU:**

i. Mzazi/ Mlezi unashauriwa kumtimizia mwanao maagizo yote yanayohitajika na hakikisha kuwa MWANAO ANAFIKA SHULENI KULINGANA NA TAREHE ILIYOAGIZWA
ii. Mzazi /Mlezi ahakikishe anaandika anuani ambayo itamuwezesha kupokea taarifa za maendeleo ya mwanae. Iweapo kutakuwa na mabadaliko yoyote ya anuani ni muhimu kutujulisha
iii. Hairuhusiwi kabisa kwa mwanafunzi kuja na nguo tofauti na zilizotajwa hapo juu
iv. Hairuhusiwi kabisa kwa mwanafunzi kubaki shuleni wakati wa likizo, hivyo kila mzazi au Mlezi amtumie mwanae nauli mapema ili kuepuka usumbufu wowote unaoweza kujitokeza.
v. Siku pekee ya kuwatembelea wanafunzi kwa muhula wa kwanza ni Jumamosi ya mwisho wa mwezi wa nane na mwezi wa kumi na kwa muhula wa pili ni jumamosi ya mwisho ya miezi ya pili na nne.

Mwanao anatakiwa kutambua kuwa nafasi aliyoipata ni nyeti na adhimu hivyo anapaswa kuitumia nafasi hiyo kwwa umakini wa hali ya juu ili baadae aweze kuwa na manufaa kwa familia, Jamii na taifa kwa ujumla

Anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ..................hadi tarehe ...............katika ofisi ya malezi. Baada ya hapo hatopokelewa kwani nafasi yake itachukuliwa na mtu mwingine ( **yaani siku 14 baada ya tarehe ya kuripoti)**
**Kwa mara nyingine tena tunampa hongera sana na kumkaribisha shuleni kwetu**

*MOTTO WA SHULE YETU NI "**DISPLINE IS SUCCESS"***
***KARIBU SANA KITOMONDO SEKONDARI.***

..............................
SEIF M. HALFAN
**MKUU WA SHULE**

NB: Tunaambatanisha nakala ya sheria za shule kwa ufahamisho kwa mzazi / mlezi wa mwanafunzi

**F: SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama inavyorekebishwa kwa Sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha , inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu. Unazingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maadishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

1. Mwanafunzi atasimama anapomsalimia mwalimu au mtu yeyote aliyemzidi umri
2. Ni marufuku kwa mwanafunzi
   a. Kutumia lugha chafu au ya kihuni popote na wakati wowote
   b. Kupeleka au kulia chakula bwenini
   c. Kufuga kucha, ndevu na nywele
   d. Kunyoa kipara
   e. Kutia dawa nywele (curl) au kujichubua ngozi ya mwili kwa madawa
   f. Kuvaa kofia shuleni au mapambo/urembo kama hereni, n.k. akiwa shuleni.
   g. Kuvaa viatu vya soli nene (ghorofa)
   h. Kuvaa kaptula, kandambili na fulana ya kukata mikono (singlet) kwenye bwalo la chakula.
   i. Hairuhusiwi mwanafunzi kuja na nguo zisizokuwa za shule.
   j. Pia haruhusiwi kutumia “chombo chochote cha umeme.
3. Atasimama kwenye mstari wakati wa kupata huduma.
4. LAZIMA mwanafunzi AWAHI NA AHUDHURIE mahali anapotakiwa katika shughuli za shule.
5. NI LAZIMA Mwanafunzi awe katika sare ya shule kwa nyakati zifiutazo:-
   (a) Anapohudhuria masomo darasani.
   (b) Anapotoka nje ya shule kwa ruksa maalumu kwa shughuli yoyote itakayomlazimu kwenda nje ya shule.
6. NI LAZIMA mwanafunzi awe ndani ya mipaka ya shule wakati wote isipokuwa akiruhusiwa kuwa njeya shule kwa ruhusa maalumu, na atapaswa kuwa na kibali (Pasi) cha maandishi.
7. Mwanafunzi lazima awe kitandani kwake wakati wa kuzima taa/kulala (lights out) saa 5.30 usiku.
8. Mwanafunzi haruhusiwi:-
   a. Kwenda kwenye nyumba za watumishi wa shule bila kibali maalum.
   b. Kuingia kwenye Ofisi za Shule – Ofisi za walimu, jikoni, na maabarabila ruhusa.
9. USAFI: Mwanafunzi anawajibika kuwa msafi na kushiriki kuyaweka mazingiraya shule katika hali ya usafi.
10. Mwanafunzi atanyoosha mkono juu na kusimama anapouliza au kujibu swali.

Mwanafunzi asipige kelele anapokuwa darasani, kwenye ‘prep’, mazingira ya shule na katikamkusanyiko wo wote

**G: MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE:-**

a) Wizi.
b) Uasherati na Ushoga.
c) Ubakaji.
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi,kubeli, na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga.

f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito/ Kupata mimba.
i) Kutoa mimba
j) Kugoma, kuchochochea nakuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama washule au watu.
k) Kukataa adhabu kwa makusudi.
l) kuwa na simu ya mkononi

GOVERNMENT OF TANZANIA

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A

TO: THE MEDICAL OFFICER

………………………………………..

………………………………………..

……………………………………….

From. The headmaster,

Kitomondo secondary school,

P.o Box 55,

Mafia.

22/05/2018

MR/MISS……………………………………………………………………………………………………………………………… ………………

(Name in full)

Please examine the above named as to her/his physical and mental fitness for being a student. The examination should include following category or sub-category (1-3), each category or sub-category of which will render the applicant ineligible in case of a defect.

Pregnancy(category 4) will also render a girl candidate ineligible for the course.

(a) Eye-light (b) Hearing (c) Limbs

(d) Speech (e) Venereal diseases (f) leprosy

(g) Epilepsy (g) S.T.I (i) neurosis

(j) Pregnancy

(J) Other serious diseases if any

…………………………………………………….

The headmaster

PART B

MEDICAL CERTIFICATE

To be completed by a Government Medical Officer

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time secondary school training course.

(a). Eye sight………………………………………………………………………….

(b). Hearing…………………………………………………………………………………………………………………….

(c). Limbs……………………………………………………………………………………………………………….

(d). Speech…………………………………………………………………………………………………………………….

(e).Venereal diseases………………………………………………………………………………………………….

(f). Leprosy……………………………………………………………………………………………………………………..

(g). Epilepsy……………………………………………………………………………………

(h). Neurosis………………………………………………………………………………………………………….

(i).Other serious diseases if any……………………………………………………………………………….

(j). Pregnancy ………………………………………………………………………………………………………………..

Medical officer's Comment…………………………………………………………………………………………….

Date……………………..Name/Signature of medical Officer …………………………………………………………….